

# Kutengeneza Jiko la Udongo Mfinyanzi “Rocket Stove”



## Vifaa vya kutengeneza

Udongo wa mfinyanzi

Mchanga

Shina la mgomba

Kipande cha metali/chuma

## **Hili ni jiko gani?**

Jiko hili lenye gharama nafuu pia ni rahisi kutengeneza. Linatumia vitu ambavyo unaweza kupata karibu na nyumbani: udongo, mchanga, mgomba, na kipanda cha metali/chuma.

## **Je, majiko haya yana faida gani?**

Kwanza, mahitaji ya kuni za kupika yatapungua kwa sababu ya ufanisi wake. Pia kwa sababu jiko hilo halitoi moshi sana, litazuia magonjwa yatokanayo na hewa chafu na moshi.

**\*Muhimu:** Sufuria ulilotengenezea jiko lako, ndilo litakalotumika kupikia. Hutaweza kupikia sufuri nyingine mbali na ile uliotengenezea, vinginevyo, tengeneza jiko linguine kwa kutumia sufuria nyingine ambayo utatumia kwenye hilo jiko. Vilevile, ni muhimu kutengeneza jiko hili pahali bila mvua kama chumba au sehemu inayotokeza.

## **Jinsi ya kutengeneza jiko hili:**

1. Tafuta na kata vipande viwili vya mgomba takribani inchi kumi na nne. Kwanza simamisha kipande kimoja cha mgomba. Ukitenganishe kipande hiki ili kipande kimoja kiwe kikubwa zaidi ya kingine kama kwenye picha.
2. Tafuta na kata kipande kimoja cha metali na urefu usawa na vipande vile vya migomba.



inavyoonekana



3. Tayarisha mchanganyiko wa udongo wa mfinyanzi na mchanga.

### Jinsi ya kuchanganya:

- Mchanga – ndoo ndogo 3 za lita kumi
- Udongo wa mfinyanzi – ndoo ndogo 1 ya lita kumi



4. Kupima mchangayiko: finyanga mchanganyiko katika umbo la mpira kisha usimame na kulidondosha umbo hilo la mpira chini. Kama umbo hilo halitaonyesha mipasuko mikubwa, mchanganyiko wako utakuwa ni mzuri.



5. Tengeneza metali au chuma bapa na uiweke katikati ya vipande viwili vya migomba uliyokata kwa ajili ya nafasi kwa kuni na hewa baadaye.



6. Chukua vipande vyako vya migomba, na kuilaza juu ya udongo mfinyanzi uliotandazwa chini. Laza kipande cha kwanza juu ya udongo mfinyanzi, kisha simamisha wima kipande kingine kama inavyoonekana kwenye picha.



7. Baada ya hapo anza kukandika kuzunguka vipande vyote viwili vya migomba.



8. Baada ya kukandika na kuvifunika vipande vyote viwili, hatua inayofuata ni kuweka sufuria juu ya kipande ulichokisimamisha wima. Kisha ukandike kunguka sufuria hiyo ili kutengeneza sehemu ya kuwekea sufuria.



9. Ni vizuri jiko lako liwe na mafaiga matatu ili kuwezesha moto kuwaka kwa ufanisi inavyoonekana kwenye picha.

10. Subiri kwa wiki mbili halafu toa taratibu vipande vya migomba vilivyokauka. Baada ya hapo jiko lako litakuwa tayari kwa kutumika.



\*Limeandikwa na Andrew "Sifuri" Clinard  
[-attikbats@gmail.com](mailto:-attikbats@gmail.com)  
[-clinard2@illinois.edu](mailto:-clinard2@illinois.edu)